# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

## RIPOTI YA KAMATI YA MAWASILIANO ARDHI NA NISHATI YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

## KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

## FEBRUARI, 2023

## YALIYOMO

**IKISIRI (ABSTRACT)** ........ 3

**SEHEMU YA KWANZA** ........ 4

UTANGULIZI ........ 4

MUUNDO WA KAMATI ........ 5

MUDA WA KAZI ZA KAMATI ........ 5

NJIA NA MBINU ZILIZOTUMIKA ........ 6

HADIDU REJEA ........ 6

**SEHEMU YA PILI** ........ 7

WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI ........ 7

WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI ........ 21

WIZARA YA MAJI NISHATI NA MADINI ........ 39

**SEHEMU YA TATU** ........ 48

HITIMISHO ........ 48

## IKISIRI (ABSTRACT)

*Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi inajukumu la kusimamia utendaji wa Wizara tatu ambazo ni: -Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi. Wizara ya Ardhi Na Maendeleo ya Makaazi pamoja Na Wizara ya Maji, Nishati na Madini. Kamati hii imeundwa kwa mujibu wa Kanuni ya 107 (1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la Mwaka 2020 na Majukumu yake yameelezwa katika Jadweli la Kwanza la Kanuni hizo. Taarifa hii inatokana na masharti ya Kanuni ya 109(15) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la Mwaka 2020 inayohusiana na Utaratibu wa Kamati za Kudumu. Kamati ilitekeleza majukumu yake Kwa Kufanya vikao Na Wizara pamoja Na Taasisi zilizo chini ya Wizara husika, Kufanya ziara za ukaguzi katika miradi ya Maendeleo na miradi ya wananchi pamoja na sehemu za kazi. Aidha Kamati ilifanya mikutano na Wafanyakazi pamoja na Wadau kwa lengo la kupokea maoni juu ya masuala mbali mbali ambayo Kamati ilikuwa inayafanyia kazi.*

*Maeneo yenye changamoto kubwa za kiutendaji Kama vile Ucheleweshaji WA Fidia ya Majengo, mazao Na miti Kwa wananchi waliopisha miradi ya Miundombinu ya Mawasiliano, Ajali za Barabarani na Uchakavu wa Miundombinu ya Usafirishaji yameainishwa. Maeneo mengine yaliyobainika kuwa Na Changamoto kubwa Ni Pamoja Na Migogoro ya Ardhi, Madeni kwa wapangaji wa Nyumba za Maendeleo pamoja na utumiaji usiofaa kwa wananchi wanaoishi katika nyumba hizo. Vile vile maeneo mengine yaliyoibuliwa kuwa na Changamoto ni pamoja na Programu ya Huduma za Maji, matatizo ya upatikanaji wa huduma bora ya Nishati ya Umeme pamoja na Madeni makubwa kwa wateja wa Shirika la Umeme Zanzibar hasa kwa taasisi za Serikali pamoja na tatizo la uvunaji wa rasilimali zisizorejesheka. Mwisho Kamati imetoa Maoni na Mapendekezo ikiwa ni pamoja na kusawazishwa kasoro ziliopo ili kufanikisha malengo na shabaha zilizolengwa ndani ya Wizara hizo na Serikali kwa ujumla.*

**RIPOTI YA KAMATI YA MAWASILIANO, ARDHI NA NISHATI YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023**

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi ni miongoni mwa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Zanzibar iliyoanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar kifungu cha 85 ya mwaka 1984 na Kanuni ya 107 (1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, (Toleo la 2020).

Majukumu ya Kamati hii yameorodheshwa kwenye Jadweli la Kwanza la Kanuni za Baraza la Wawakilishi kama ifuatavyo:

a) Kufatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia;
b) Kufatilia utekelezaji wa sera na mipango ya Wizara husika kwa kadri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji kwa Bajeti na hotuba nyengine za Wizara ilizotoa katika Baraza;
c) Kufatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na miradi ya wananchi ya Wizara husika;
d) Kuchunguza na kufatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha;
e) Kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka;
f) Kushughulikia miswada ya sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika;
g) Kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufuatilia utekelezaji wa ahadi hizo;
h) Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati mbali ya majukumu yake yaliyoainishwa kwa mujibu wa Kanuni lakini pia ina jukumu la kufatilia utekelezaji wa wizara tatu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ikiwemo Mashirika, Mamlaka na Vitengo vilivyomo ndani ya Wizara hizo. Wizara zinazosimamiwa na Kamati hii ni: -

1. Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi

2. Wizara Ardhi na Maendeleo ya Makaazi
3. Wizara ya Maji, Nishati na Madini

## 1:1 MUUNDO WA KAMATI

Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati imeundwa na Wajumbe Sita (6) na makatibu wawili (2), orodha ya Wajumbe na Makatibu ni kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe Yahya Rashid Abdullah | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe Hudhaima Mbaraka Tahir | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe Mussa Foum Mussa | Mjumbe |
| 4. | Mhe Hussein Ibarahim Makungu | Mjumbe |
| 5. | Mhe Kombo Mwinyi Shehe | Mjumbe |
| 6. | Mhe Bahati Khamis Kombo | Mjumbe |
| 7. | Ndg. Rahma Kombo Mgeni | Katibu |
| 8. | Ndg. Himid Haji Choko | Katibu |

## 1:2 MALENGO YA KAMATI

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ilifanya kazi zake kwa kufata malengo yafuatayo:

1. Kufatilia maagizo yaliyotolewa katika ripoti ya Kamati ya mwaka 2021/2022.

2. Kufatilia ahadi za Serikali zilizotolewa katika Mkutano wa Bajeti wa Mwaka 2022/2023.

3. Kufatilia utekelezaji wa Bajeti (kwa kazi za Kawaida na kazi za Maendeleo) kwa mwaka 2022/2023.

4. Kufatilia ukusanyaji wa mapato katika vitengo vya Serikali pamoja na kufanya ziara kwa Taasisi zake.

## 1:3 MUDA WA KAZI ZA KAMATI

Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ilifanya kazi zake kama ifuatavyo: -

1) Pemba kuanzia tarehe 09/08/2022 hadi tarehe 13/08/2022,
2) Unguja kuanzia tarehe 15/08/2022 hadi tarehe 19/08/2022,

3) Pemba kuanzia tarehe 31/10/2022 hadi tarehe 40/11/2022
4) Unguja kuanzia tarehe 07/11/2021 hadi tarehe 11/11/2022
5) Pemba kuanzia tarehe 23/01/2023 hadi tarehe 27/01/2023
6) Unguja kuanzia tarehe 30/01/2023 hadi tarehe 03/02/2023

## 1.4 NJIA NA MBINU ZILIZOTUMIKA

Katika kuhakikisha Kamati inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kwa mujibu wa Kanuni, Kamati ilitumia njia na mbinu mbali mbali ikiwemo: -

*(i)* Kufanya vikao na Wizara pamoja na Taasisi zilizo chini ya Wizara husika kwa lengo la kupata taarifa juu mambo au maswala mahsusi ambayo Kamati ilipenda kupata taarifa zake kutoka kwa watendaji wa taasisi hizo.

*(ii)* Kufanya ziara za ukaguzi katika miradi ya Maendeleo, sehemu za kazi na sehemu nyengine ambazo kwa namna moja ama nyengine zinahusika na utekelezaji wa majukumu ya Wizara husika.

*(iii)* Kufanya mikutano na Wafanyakazi pamoja na Wadau kwa lengo la kupokea maoni juu ya masuala mbali mbali ambayo Kamati ilikuwa inayafanyia kazi.

Kamati imebaini kwamba njia hizi ilizotumia zimeleta manufaa makubwa kwani, kutokana na njia hizo imeweza kufahamu mafanikio na changamoto zinazoikabili Wizara na Idara husika katika utekelezaji wa majukumu yao.

## 1.5 HADIDU REJEA

Katika Utekelezaji wa kazi kwa mwaka 2022/2023 Kamati ilitumia hadidu rejea zifuatazo; -

a) Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984.
b) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977
c) Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la Mwaka 2020.
d) Hansard za Baraza za Mwaka 2022/2023,
e) Hotuba za Bajeti za Wizara zinazosimamiwa na Kamati hii

## SEHEMU YA PILI

## WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI

### 2.0 MUUNDO WA WIZARA.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ni miongoni mwa Wizara za ambayo inaundwa na Idara nne, pamoja na Taasisi Saba zinazojitegemea, Idara hizo ni: -

i. Idara ya Utumishi na Uendeshaji,
ii. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti,
iii. Idara ya Mawasiliano
iv. Ofisi Kuu Pemba.

Taasisi zinazojitegemea ni

i. Shirika la Bandari,
ii. Shirika la Meli, Mamlaka ya Usafiri Baharini,
iii. Mamlaka ya Viwanja vya Ndege,
iv. Wakala wa Mkonga wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano,
v. Wakala wa Barabara, na
vi. Wakala wa Karakana Kuu ya Magari.

### 2.1 MAJUKUMU YA WIZARA

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi imepewa jukumu la kusimamia Sekta ya Usafirishaji na Mawasiliano Zanzibar. Sekta ya Usafirishaji inajumuisha usafiri wa Nchi kavu, Anga na Baharini. Sekta ya Mawasiliano inajumuisha usimamizi wa miundombinu na huduma za Mawasiliano Zanzibar.

### 2.2 PROGRAMU ZA WIZARA

Kwa kuzingatia Majukumu ya Wizara, kwa mwaka wa fedha 2022/2023,
Wizara ina programu kuu tatu (3) zenye Programu ndogo tano (5) kama zifuatazo: -

1. PROGRAMU YA USAFIRISHAJI
2. PROGRAMU YA TEKNILOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA)
3. PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI

### 2:2:1 MAENEO YALIYOTILIWA MKAZO NA KAMATI

Katika Ripoti hii kwa makusudi kabisa katika Wizara hii, Kamati ilijikita zaidi kufuatilia miradi mikubwa ya Kimkakati pamoja na azma ya Serikali hivi sasa ya kuifungua Pemba kiuchumi na kuifanya kuwa kituo mahsusi cha uwekezaji kwa kufuatilia kwa kina uimarishaji wa miundombinu ya Barabara, Bandari na Uwanja wa Ndege. Shughuli hizo moja kwa moja zinaingia katika Programu ya Usafirishaji pamoja na Programu ya Uendashaji na Uratibu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

### 2:2:2 MIRADI YA MAENDELEO YA WIZARA

#### 2:2:2:1 Mradi wa Ujenzi wa Barabara za Mjini Unguja kilomita 103.9

Kamati imebaini kwamba Mradi huu unajumuisha ujenzi wa barabara za Mjini Unguja zenye urefu wa km 103.9 kwa kiwango cha lami. Aidha, unajumuisha ujenzi wa barabara za juu (Fly Over) katika eneo la Amani na Mwanakwerekwe "round about" ili kupunguza msongamano wa magari katika maeneo hayo. Mradi huu umeanza rasmi tarehe 01 Disemba, 2022 na unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi 36.
Utafiti wa Kamati ubebaini kwamba hadi Disemba 2022, Mkandarasi ameanza kazi ikiwemo kujenga kambi, kuleta vifaa pamoja na kuandaa michoro ya barabara sita (6) ambazo ni kipaumbele cha mwanzo na baadhi ya barabara ujenzi ulikuwa unaendelea na kwa ujumla wake umefikia asilimia **0.3%** za utekelezaji.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

I. Kamati inaishauri Wizara kuongeze kasi ya ufuatiliaji na usimamizi wa mradi huu ili kuhakikisha Mkandarasi anakafanya kazi kwa utaratibu na kasi inayohitajika na hatimae kukabidhi mradi kwa muda uliopangwa na kupunguza kadhia kubwa ya msongomano wa magari katika maeneo ya mjini.

#### 2:2:2:2 Mradi wa Ujenzi wa Barabara za ndani zenye jumla ya kilomita 275.9 Unguja na Pemba

Mradi huu ulianza rasmi tarehe 26 Machi, 2022 na unatarajiwa kukamilika ndani ya kipindi cha miezi 40. Kamati imearifiwa kwamba Mradi huu unaendelea na hatua mbalimbali za ujenzi zimefikiwa kwa Upande wa Unguja

ambapo hadi kufikia mwishoni mwa mwezi wa Disemba, 2022, Mradi huu umefikia asilimia **11.5%** ya utekelezaji. Kwa upande wa Pemba kazi hii ilitegemewa kuanza mwaka huu wa 2023 baada ya kupita mvua za masika na kukamilika kwa kazi za design.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1) Wizara iharakishe Mradi wa Ujenzi wa barabara za ndani ili kuwapatia wananchi huduma bora za barabara mijini na vijijini na pia kuendana na kasi ya Serikali ya Awamu ya nane ya kuwaletea maendelea makubwa wananchi.

2) Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha utekelezaji wa Mradi unakwenda sambamba kwa upande wa Unguja na Pemba na hatimae ukamilike kwa muda uliopangwa ili wananchi wa watumuie moundombinu bora na iliyo salama lakini pia kufikiwa azma iliyokusudiwa na Serikali ya Awamu ya Nane.

**2:2:2:3 Mradi wa Ujenzi wa Barabara Kuu nne Unguja na Pemba.**
Mradi huu unajumuisha Barabara ya Tunguu - Makunduchi kilomita 48.5, Fumba – Kisauni kilomita 12, Chake – Mkoani kilomita 43.5 na Barabara ya Wete – Chake kilomita 22.1. Utekelezaji wa miradi hii ni kama ifuatavyo: -

**a) Ujenzi wa Barabara ya Wete - Chake kilomita 22.1.**
Kamati imejulishwa kwamba utekelezaji wa mradi huu ni miezi 30 na ulianza rasmi mwezi wa Febuari 2022 na unatarajiwa kukamilika mwezi Julai 2024.
Kamati ilitembelea Mradi huu katika mizunguko yote ya Kazi za Kamati na kubaini kwamba hadi kufikia mwezi wa Disemba, 2022 hatua ya ujenzi iliyofikiwa ni usafishaji wa barabara kwa urefu wa kilomita 10.7 pamoja na kutengeneza tuta la barabara kilomita 6.0 na hadi tunaandaa ripoti hii umefikia asilimia **8.8%** ya utekelezaji.

**Changamoto**

Kamati imebaini kwamba licha ya ujenzi huu kusua sua, mkandarasi tayari ameongeza vifaa na rasilimali watu ili kuongeza kasi na kufanya kazi kwa mpangilio unaotakiwa, lakini mradi umekumbwa na changamoto kubwa ya Fidia kwa Nyumba, miti na Mazao yaliyoathiriwa kwa kupisha ujenzi huo.

**MAONI NA USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano, na Usafirishaji ihakikishe inashirikiana na taasisi zote kuharakisha utaratibu wa mzuri wa ulipwaji wa fidia kwa wale wote walioathirika ili kuweza kupisha mradi huu wa kimkakati wa maendeleo kwa wakati na thamani halisi kulingana na mfumko wa bei.

2. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara hii iwapo kunakuwa na uhakika wa fedha, ni vyema kufikiria njia mbadala hata kwa kukopa katika taasisi zake za Kifedha badala ya kusubiri michakato na urasimu uliopo katika baadhi ya taasisi za kiserikali ili kuendana na muda wa mradi na thamani kulingana na wakati ili kuwaondolea minung'uniko wananchi.

3. Kamati inahimiza umakini, uadilifu, uaminifu na mashirikiano kwa taasisi za Serikali katika miradi kama hii ya kimkakati wakati wa kutathmini rasilimali ili kuhakikisha kila muathirika analipwa kwa mujibu wa mali yake na wakati uliopo na kuepusha changamoto zinazojitokeza katika miradi hii ya kimkakati.

**b) Ujenzi wa Barabara ya Tunguu - Makunduchi kilomita 48.5, Fumba – Kisauni kilomita 12 na barabara ya Chake – Mkoani kilomita 43.5.**

Hadi Kamati inapokea taarifa za Miradi hii, Mkandarasi alikuwa akisuburi kukamilika kwa taratibu za utoaji wa fedha kutoka kwa Mfadhili ili aweze kuanza kazi.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji Wizara kuharakisha utekelezaji wa miradi kama hii ya Kimkakati ile kwenda sambamba na dhamira na kasi ya Serikali ya Awamu ya Nane ya kuwaletea maendeleo ya haraka wananchi wake.

**2:2:2:4 Mradi wa Uimarishaji wa Uwanja wa Ndege wa Pemba**

Miongoni mwa hatua za Serikali za kuifungua Pemba kiuchumi ni Uimarishaji wa uwanja wa ndege wa Pemba ili ukidhi mahitaji ya ongezeko la abiria na

wakati wa sasa kwa kuazimia kuutanua uwanja huo pamoja na jengo jipya la kusubiria abiria.
Utafiti wa Kamati umebaini kwamba hatua za ujenzi zitaanza baada ya kukamilika hatua za "Mobilization" kwa mjenzi huyo na Serikali kukamilisha ulipaji wa fidia kwa wananchi ambao maeneo yao yataathiriwa na ujenzi huo.

**Changamoto:**
Kamati kwa makusudi ilitembelea Uwanja huo kufuatilia jinsi wafanyakazi pamoja na taasisi zinazotoa huduma walivyojipanga kuikabili hatua hiyo mpya kwa maendelea ya Pemba na kugundua Changamoto mbali mbali ikiwemo: -

a) Kukosekana kwa bajeti ya kutosha ya uendeshaji wa shughuli za uwanja wa Ndege kwa upande wa Pemba.
b) Upungufu wa Mashine za ukaguzi wa mizigo (X-RAY MACHINE) ambapo kwa sasa ni mashine mbili tu zinazofanya kazi.
c) Kutokuwekwa uzio eneo la kilomita moja lililobakia.
d) Kutokuwa na gari ya uhakika la zima moto na uokozi.
e) Ukosefu wa huduma za kibenki.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**
1. Wizara ihakikishe inaongeza Mashine za ukaguzi wa mizigo (X-RAY MACHINE) ikiwa ni hatua moja wapo ya kuimarisha usalama kiwanjani hapo.
2. Wizara ihakikishe inaweka uzio eneo la kilomita moja lililobakia.
3. Wizara ishirikiane na Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum na kuangalia namna ya kukipatia kiwanja hicho gari la zimamoto la uhakika.
4. Wizara ihakikishe inaimarisha ofisi zote zilizopo Katika Uwanja wa ndege wa Pemba zitakazowezesha taasisi zote zinazotoa huduma kiwanjani hapo kufanya shughuli zao kwa ufanisi mzuri kulingana na wakati wa sasa ikiwemo mtandao wa intanet na huduma za kibenki ili kuweza kufanikisha huduma zinazotolewa kiwanjani hapo kukidhi haja.

**2:2:2:5 Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC)**

Kamati imebaini kwamba katika kutekeleza Programu ya Usafirishaji, Shirika la Bandari limeendelea na mkakati wake wa kuimarisha miundo mbinu ya Bandari zake ikiwemo Bandari ya Mkoani, Bandari ya Malindi, Bandari ya Shumba Mjini na Bandari ya Mkokotoni.

A. **Bandari ya Malindi**

Kamati ibebaini kwamba Bandari ya Malindi inakabiliwa na tatizo la uhaba wa nafasi na kupelekea msongamano wa makontena katika Bandari hiyo, ambapo hadi kufikia Disemba 2023, Shirika limefanya yafuatayo; -

a) Uchimbaji wa mchanga katika Gati nambari 3 kwa lengo la kuongeza kina cha maji. Lengo ni kupata eneo jengine la kuegeshea meli kwa ajili ya kupunguza kukaa muda mrefu kusubiri huduma.

b) Ujenzi wa eneo la kuwekea makontena katika eneo la Bwawani ilikuondosha kazi ya upakuaji wa mizigo katika makontena ndani ya eneo la Bandari na kupunguza msongamano wa mizigo bandarini.

**Ubinafsishaji wa Bandari ya Malindi.**

Kamati imebaini kwamba katika kuimarisha huduma za Bandari ya Malindi, Serikali imepanga kumpa muendeshaji wa Bandari hii na kwa sasa Serikali na muendeshaji huyo wapo katika mazungumzo ya mwisho kabla ya kufungiana mikataba.
Kamati inadhani hatua hii inaweza kuongeza ufanisi wa utendaji wa bandari hii.

**Changamoto Katika Bandari ya Malindi.**

a) Ufinyu wa eneo la kuhifadhia makontena
b) Udogo wa gati
c) Ucheleweshaji wa utoaji wa mizigo.
d) Huduma zisiziridhisha kwa maeneo ya abiria
e) Utaratibu usioridhisha wa Uingiaji na utokaji wa magari ya mizigo kutoka nje ya Zanzibar.

B. **Bandari ya Mkoani**

1. Kamati imeshuhudia kazi za kuimarisha Bandari ya Mkoani kwa ajili ya kuhudumia meli za Makontena. Uimarishaji huo umelenga eneo la kuhifadhia makontena, pamoja na Kujenga upya njia ya wapita kwa miguu. Hadi kufikia Disemba, 2022 kazi imefikia asilimia **60%** ya utekelezaji na kazi zilizofanyika ni kama ifuatavyo; -

2. Ukarabati wa gati kwa kuondosha mipasuko, nondo zilizooza na kubadilisha viguzo vya kufungia meli katika gati, ili kuifanya iwe imara zaidi na kutumika kwa muda mrefu.
3. Uwekaji wa wa zege katika sehemu ya kuhifadhia makontena (Container Yard), sambamba na ujengaji wa nguzo za ukuta (fence) katika eneo hilo
4. Ujenzi wa ukuta wa mawe katika eneo la Baharini kwa ajili ya kuzuia mmong'onyoko kwenye sehemu ya kuweka makontena.
5. Undoshwaji wa njia ya zamani ya waenda kwa miguu iliyokuwepo sehemu ya katikati ya barabara umekamilika na uwekaji wa zege jipya katika sehemu hiyo unaendelea, ili kuimarisha njia hiyo kwa lengo la kupita magari na vyombo vyengine.
6. Ujenzi wa njia mpya ya wanaotembea kwa miguu ambayo itakuwa na kipaa cha kuzuia abiria kupigwa na mvua au jua inaendelea.

### C. Bandari ya Mkokotoni

Shirika katika mwaka wa fedha 2022/2023 ilipanga kujenga njia ya wapita kwa miguu na jengo la kupumzikia abiria lenye uwezo wa kuhifadh abiria 250 ikiwa ni muendelezo wa kuimairisha Bandari hiyo. Hadi kufikia Disemba 2022 shughuli hizo zimefikia asilimia **90%.**

Aidha Kazi ya kutengeneza Apporaching channel ili kuruhusu meli kuingia bandarini ipo katika hatua za kufungiana Mkataba na Kampuni ya Costal dredging na inatarajiwa kuchukua miezi mitatu.

Kukamilika kwa mradi huu kutaiiwezesha Wizara kuanzisha safari za kuhudumia meli za abiria baina ya Mkokotoni na Pemba kupitia bandari ya Mkokotoni lengo ni kuipinguzia Bandari ya Malindi msongamano wa abiria na mizigo.

### D. Bandari ya Mangapwani

Serikali ina mpango wa ujenzi wa Bandari Jumuishi ya kuhudumia wa makontena na kichele, mafuta na gesi na Chelezo cha kufanyia matengenezo Vyombo vya baharini. Kazi zilizofanyika hadi kufikia sasa ni: -

a) Kutayarisha Mpango Mkuu (master plan) ambao umeshakamilika na kukabidhiwa kwa Serikali.

b) Kufanya mazungumzo na Muelekezaji mwenye nia ya kuwekeza katika ujenzi wa Bandari ya Makontena na mizigo, ambapo tayari Serikali ipo katika hatua za awali za uandaaji wa mkataba na muekezaji huyo.
c) Aidha, kwa upande wa Mafuta na gesi wameshajitokeza wawekezaji watano (5) ambapo kwa sasa Wizara inaendelea kupitia nyaraka zao.

**E. Bandari ya Shumba Mjini**

Shirika lipo katika hatua za ujenzi wa Bandari ya kuhudumia abiria na mizigo ambayo inatarajiwa kuhudumia meli zenye uzito wa tani 2,000. kamati imebaini kwamba Mkandarasi alikabidhiwa eneo (site) mwezi Juni, 2022 kwa ajili ya kuanza hatua za ujenzi na ujenzi huo unaotarajiwa kuchukua miezi 11na hadi kufikia Disemba 2022,
Hadi kufikia Disemba 2022 Kwa ujumla kazi hii imefikia asilimia **30%** ya utekelezaji wake kwa kufanya mambo yafuatayo zilizofanyika ni pamoja na: -

a) Kusafisha eneo na kujenga uzio ambao utasaidia kuzuia wananchi wasiweze kuingia katika eneo la ujenzi (Mobilization and Site establishment).
b) Kufanya utafiti wa maumbile ya ardhi katika eneo la ujenzi kwa lengo la kufahamu namna eneo la juu na eneo la Baharini linavyoendana kwa ajili ya kutengeneza mchoro ambao utatoa picha halisi ya ujenzi wa gati katika eneo hilo (Topography and Bathymetric Surveys);
c) Uchimbaji na utafiti wa udongo na mwamba wa Baharini (Geotechnical Investigation) kwa lengo la kutambua aina ya udongo uliopo katika eneo hilo, ili kuandaa mchoro (Structure) utakao endana na aina ya udongo uliopo eneo hilo.
d) Aidha, Shirika limeshapokea mapendekezo ya mchoro wa awali kutoka kwa Mkandarasi na upo katika hatua ya kupitiwa na Uongozi wa Wizara kabla ya kuruhusu Mkandarasi kuanza ujenzi.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1. Wizara ihakikisha hatma njema kwa wafanyakazi wa Bandari ya Malindi wakati inaelekea katika kukabidhiwa kwa mwekezaji wa kuendesha bandari hiyo.
2. Wizara na Serikali kwa ujumla iangalie maeneo ya Bandari ya Malindi yanayoweza kutolewa katika Mpango wa uhifadhi wa Mji Mkongwe (UNESCO) ili kuweza kuyatumia kwa kuyakarabati na kuongeza nafasi katika maeneo ya Bandari.

3. Kamati inashauri Wizara kupitia Bandari ya Malindikuimarisha huduma katika maeneo yaote hasa katika eneo la kushukia abiria ili kuondosha msongamano uliopo sasa.
4. Pia, Kamati inaendelea kushauri kuwekwa utaratibu maalum utakaozingatia matumizi ya eneo la watu mashuhuri (VIP).
5. Kamti inaishauri Wizara kupitia Shirika la Bandani kuliangalia kwa kina suala la uingiaji na utokaji wa magari ya mizigo kutoka nje ya zanzibar, kwani kumekua na malalamiko ya wadau kuhusiana na kutumika vibaya magari hayo na kuikoseha serikali mapato.
6. Wizara ijipange mapema kufikiria kulipa fidia na kuondoa kituo cha mafuta kiliopo Bandari ya Mkoani ambacho kipo karibu mno na Sehemu ya kuhifadhia Makontena.
7. Wizara ishirikiane na Serikali ya Wilaya ya Mkoani ili kutafuta suluhisho la Kituo cha gari za abiria ndani ya bandari ya Mkoani ambacho kinaweza kuleta muingiliano na usumbufu mkubwa baada ya kukamilika mradi wa kuimarisho bandari hiyo.
8. Wizara iharakishe ujenzi wa miradi ya bandari za Mangapwani, Mkokokotoni na Fumba Mjini inafanikiwa kama ambavyo Serikali inavyokusudia, kwani kukamilika kwake kutasaidia kupunguza msongamano wa abiria na mizigo uliopo katika bandari mama ya Malindi.

### 2:2:2:6 Wakala wa Barabara Zanzibar

Wakala wa Barabara taasisi yenye jukumu la kujenga, kutunza na kuzifanyia matengenezo barabara mbalimbali za Unguja na Pemba ili ziweze kupitika muda wote. Kwamujibu wa taarifa ya Wizara, hadi kufikia Disemba, 2022, Wakala wa Barabara imefanikiwa kufanya matengenezo kwa kusawazishwa ili kuweza kupitika katika eneo lenye urefu wa mita 350 katika barabara ya Jumbi - Tunguu Round about. Aidha, kazi za uzibaji mashimo kwa barabara mbali mbali za lami zimefanyika Unguja na Pemba lakini ameshindwa kufanya shughuli mbali mbali alizojipangia kutokana na ukosefu wa fedha kutoka serikalini.

**Changamoto/ Shughuli ambazo Wakala wa Barabara ameshindwa kuzifanya**

a) Kushindwa Kujenga barabara mbalimbali Unguja na Pemba zikiwemo barabara za Unguja Ukuu – Uzi Ngambwa, Tumbatu, Kiboje - Ukuchuni, Micheweni- Msasani na Kijangwani – Birikau.

b) Kushindwa Kufanya Matengenezo mbalimbali ya barabara Unguja na Pemba ikiwemo Chanjamjawiri – Tundauwa, Chanjani – Pujini, Mizingani – Wambaa na Kenya- Chambani

c) Kushindwa Kujenga misingi 26 ya maji ya mvua

d) Kushindwa Ujenzi wa Madaraja na Makalvati Unguja na Pemba ikiwemi Machui, Chamanangwe na Vitongoji

e) Kushindwa kufanya Kazi za utunzaji wa barabara katika barabara nyingi za Unguja na Pemba.

f) Kushindwa Kuweka Miundombinu ya usalama barabarani katika baadhi ya barabara.

**2:2:2:7 Ziara ya Kamati Tanzania Bara**

Kamati kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa vipindi kadhaa ilikwenda Tanzania Bara kwa ajili ya kujifunza masuala mbali yahayohusu utekelezaji wa Wizara hiyo kwa lengo la kupata taaluma na baadae kuishauri ipasavyo Serikali hasa katika Masuala ya Bandari, Mawasiliano, pamoja na Taasisi mbali mbali za Jamhuri ya Muungano zenye ofisi zao hapa Zanzibar.

Kamati ilibahatika kutembelea Mkoa wa Pwani na kushuhudia Ujenzi wa Barabara ya Kibiti- Nyamisati yenye urefu wa Kilomita 42. Kamati ilishuhudia barabara hiyo ya kiwango cha kifusi ikisheheni alama za barabarani, mitaro ya maji, madaraja na mipaka ya hifadhi ya barabara.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI.**

1. Serikali ihakikishe inampatia fedha za kutosha na kwa wakati Wakala wa Barabara ili aweza kutekeleza majukumu yake kwa muda uliopangwa.

2. Wizara isawazishe Mifumo na taratibu za manunuzi ili kumuwezesha Wakala wa Barabara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi unaohitajika.

3. Wizara ihakikishe inapofanya miradi ya barabara mikubwa na midogo inazingatia kujumuisha uwekaji wa alama, mitaro ya maji, na alama za hifadhi ya Barabara ili kuepusha ajali na uvamizi wa maeneo yake.

4. Wizara ihakikishe inaweka Alama za barabarani (Road Sign) na Michoro ya Barabarani (Road mark) ili ziweze kuwaongoza vyema madereva na watumiaji wote wa barabara kwa lengo la kuepusha misongomano hasa katika makutano ya barabara na pia kujikinga na ajali.

5. Wizara ifikirie kuzijenga upya barabara kongwe kwani hivi sasa zinaonekana kumaliza muda wake wa matumizi (life Spain) ili kukabiliana na ongezeko pamoja na uzito wa magari kwa wakati wa sasa pamoja na mashimo yanayoendelea kuibuka kila mara.

6. Kamati inaishauri Wizara kuwa na mipango ambayo itaweza kutekelezeka kulingana na bajeti iliyopo na kuachana na tabia ya kuweka malengo mengi ambayo baadae tunashindwa kuyakamilisha hasa katika miradi ya barabara.

7. Kamati kwa mara nyengine tena isaisisitiza Wizara kupitia Wakala kuziba mashimo katika barabara zote kwa Unguja na Pemba ili kuondosha usumbufu unaojitokeza na kupunguza ajali zitokanazo na mashimo hayo.

### 2:2:2:8 Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani.

Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani ina jukumu la kudhibiti usalama wa watumiaji wa barabara pamoja na utoaji wa huduma za usafiri wa barabarani.

**Changamoto**

1. Kamati ilitembelea Ofisi za Mamlaka hiyo Unguja na Pemba na kubaini changamoto zifuatazo: -

2. Kukosekana kwa jengo lenye vifaa vya kisasa vya ukaguzi wa vyombo vya moto.
3. Uhaba wa vitendea kazi kama Gari kwa matumizi ya ofisi hasa kwa upande wa Pemba.
4. Uhaba wa wataalamu hasa katika kada ya upasishaji wa vyombo na upasishaji wa madereva.
5. Kutokuruhusiwa kutumia asilimia ya mapato yanayokusanya kwa ajili ya uendeshaji waTaasisi.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1) Wizara ihakikishe inazisimamia ipasavyo Sheria, Kanuni na Miongozo ya Usalama wa Barabarani ikiwa ni njia moja wapo ya kujikinga na ajali zinazoendelea kuangamiza nguvu kazi ya taifa.

2) Wizara ihakikishe inaweka Alama za barabarani (Road Sign) na Michoro ya Barabarani (Road mark) ili ziweze kuwaongoza vyema madereva na watumiaji wote wa barabara kwa lengo la kuepusha misongomano hasa katika makutano ya barabara na pia kujikinga na ajili.

3) Kamati inaishauri Wizara kukaa pamoja na taasisi zote zinazosimamia taa za kuongozea watumiaji wa barabara na kukubaliana kuwa na msimamizi mmoja ili kuongeza uwajibikaji badala ya hali iliyopo hivi sasa.

4) Wizara iwe na utaratibu unaofahamika wa vibali vya njia na matumizi ya Barabara kwa gari zote zinazotokea nje Zanzibar zikiwa tayari na mizigo na kuisambaza katika maeneo ya Zanzibar.

### 2:2:2:9 Shirika la Meli Zanzibar

Shirika la Meli Zanzibar limepewa jukumu la kuendesha meli zote za Serikali pamoja na kutoa huduma za uwakala kwa meli za Kigeni zinazoingia katika bandari za Zanzibar.
Kamati imeripotiwa kwamba Shirika la Meli, limefanikiwa kuuza meli zake mbili (2) ambazo ni MV Maendeleo kwa thamani ya USD 230,000 na MT. Ukombozi kwa thamani ya USD 251,000. AiUtafiti wa kamati umebaini kuwa Meli ya MV Mapinduzi 11 haikuuzwa kutokana na ha wazabuni kutofikia bei elekezi iliyowekwa na mtathmini Mkuu wa Serikali.

**Changamoto**

1) Serikali kuchelewa kufanya Maamuzi ya kuiuza Meli ya MV Mapinduzi II.

2) Shirika kuchelewa kufanyiwa kazi Ushauri wa Kamati ya Mawasiliano ya Baraza la Wawakilishi, Viongozi na wadau wengine kuhusiana na kuiuza Meli ya MV Mapinduzi II hadi kupelekea kushuka thamani kulingana na wakati uliopo.

**MAAGIZO, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1) Serikali inapofanya manunuzi ya vyombo vya usafiri iangalie mahitaji halisi ya wakati uliopo ikiwa ni pamoja na kutafuta vifaa ambayo vitakuwa na unafuu wa kuuzika au kuingia ubiya pale itakapo hitajika.
2) Kwa kuwa serikali ipo katika mpango wa kuitengeneza meli ya MV Mapinduzi II, Kamati inashauri matengenezo hayo kufanyika kwa haraka ili kuondosha gharama zisizokuwa za lazima na kupunguza changamoto ya uhaba wa usafiri iliopo sasa.

**2:2:2:10 Mamlaka ya Usafiri Baharini (ZMA)**

Mamlaka ya Usafiri Baharini ina jukumu la kusimamia usafiri wa baharini ikiwemo kusimamia usalama na ulinzi wa vyombo vya baharini, kusimamia shughuli za ukaguzi na usajili wa meli, utoaji wa leseni kwa vyombo vidogo vidogo, utoaji wa leseni za manahodha na wahandisi wa vyombo vidogo vidogo, utoaji wa hati na vitambulisho vya mabaharia, kusimamia shughuli za upakiaji wa abiria katika bandari za Zanzibar, kudhibiti uchafuzi wa mazingira ya baharini na utekelezaji wa kanuni ya kimataifa ya ulinzi wa meli na bandari (ISPS Code).

**Changamoto**

a) Kutokufuatwa kwa taratibu za safari za meli hasa Unguja/Pemba/ Tanga na kupelekea abiria kukaa muda mrefu bandarini kusubiri safari hizo.

b) Ulanguzi wa tiketi za safari za meli kati ya Unguja/Dar es Salaam/Pemba na Tanga.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1) Kamati inaishauri Mamlaka kuhakikisha wamiliki wote wa Vyombo vya Usafiri Baharini hasa Meli za abiria kuhakikisha wanafuata taratibu za usafiri wa baharini.

2) Mamlaka pia ifuatilie Mienendo ya Safari za Meli za Abiria na mizigo badala ya kuelekeza nguvu kubwa katika usajili wa meli kwani abiria wamekuwa wakipata usumbufu mkubwa hasa safari za Unguja/Pemba/Tanga.

3) Wizara ihakikishe Kampuni zote za meli za abiria zinatumia mifumo ya kisasa katika uuzaji wa tiketi ili kuzuia ulanguzi wa tiketi Bandarini.

4) Kamati inaishauri Mamlaka kuendelea kutoa taaluma kwa wananchi kuhusiana na kukata tiketi katika maeneo rasmi yaliyosajiliwa na sio mikononi mwa walanguzi.

5) Mamlaka ihakikishe usalama wa abiria na mizigo wakati wote wa safari ili kuepusha athari zinazoweza kujitokeza.

## WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI

### 3.0 UTANGULIZI

Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi ni miongoni mwa Wizara 16 zilizoundwa kupitia "Legal Notice No.14" ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ya tarehe 12 Disemba, 2020 ambayo imeainisha Wizara, Majukumu ya Wizara na Taasisi zitakazounda Wizara husika. Aidha, Wizara hii ina dhamana ya kuhakikisha kwamba wananchi wote wa Zanzibar wanapata makaazi bora, salama na nafuu.

### 3.1 MUUNDO WA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI

Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi inajumuisha Idara na Taasisi zifuatazo: -

i. Idara ya Mipango Sera na Utafiti,
ii. Idara ya Uendeshaji na Utumishi,
iii. Ofisi Kuu Pemba,
iv. Kamisheni ya Ardhi (COLA),
v. Mahakama ya Ardhi,
vi. Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali,
vii. Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA) na
viii. Shirika la Nyumba Zanzibar (ZHC)

Aidha, Wizara ina Bodi Tendaji (Executive Boards) tano (5) ambazo ni:-

i. Bodi ya Uhaulishaji Ardhi,
ii. Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba,
iii. Bodi ya Kondominio,
iv. Bodi ya Usajili wa Wakandarasi na
v. Bodi ya Usajili wa Wahandisi, Wasanifu na Wakadiriaji Majengo.

### 3.2 PROGRAMU ZA WIZARA

Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi inatekeleza majukumu yake kupitia Programu Kuu 2 ambazo ni;

**PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI.**

**PROGRAMU YA USIMAMIZI WA ARDHI NA MAKAAZI**

### 3.2:1 PROGRAMU KUU: UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA ARDHI

Programu hii ina jukumu la kuratibu utekelezaji wa kazi za Wizara na inajumuisha Programu ndogo tatu ambazo zinatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Idara ya Utumishi na Uendeshaji na Afisi Kuu Pemba.

**Changamoto zinazoikabili Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi**

a) Uhaba wa bajeti ambao hupelekea kukwamisha juhudi za utekelezaji wa majukumu ya Wizara.
b) Upungufu wa wataalamu katika fani za kitaalamu kupitia Taasisi mbali mbali zilizo chini ya Wizara hali ambayo inakwaza katika utekelezaji wa kazi za Wizara.
c) Ukosefu wa hatimiliki kwa nyumba zinazomilikiwa na wizara Pamoja na Taasisi zake.

**MAONI , USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

i. Kamati inaomba Serikali kupitia Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kuongezwa bajeti ya Wizara ili kuweza kutatuliwa na kutekelezwa majukumu ya Wizara kwa ufanisi kama ilivyokusudiwa ili kuondokana na mazowea ya kutofikiwa malengo ya Wizara kwa kila mwaka wa fedha hali ambayo inarudisha nyuma juhudi za Wizara.

ii. Kamati inaendelea kusisitiza kuchukuliwa hatua suala la upatikanaji wa wafanyakazi wa fani za kitaalamu katika Wizara kupitia idara zake ili kuweza kutekelezeka vyema majuku yaliyokusudiwa.

iii. Kamati kwa mara nyengine tena inaisisitiza Wizara kuhakikisha majengo yao yote yanapatiwa hatimiliki lakini pia kutoa ushauri kwa Serikali juu ya umuhimu wa kuwepo hatimiliki kwa majengo yote yanayomilikiwa na Serikali ili kupunguza changamoto ya uvamizi na migogoro baina ya Serikali na wananchi.

### 3.2:1:1 PROGRAMU NDOGO YA IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Programu hii ndogo ina jukumu la kutekeleza shughuli za kuratibu/ kuandaa Mipango na Miongozo ya Kisera ya utekelezaji wa kazi za Wizara, kuratibu uandaaji na mapitio ya Sera, Sheria, Bajeti, ufatiliaji na kufanya tathmini ya kazi za Wizara na miradi ya Maendeleo pamoja na kuendeleza tafiti kwa ajili ya kuimarisha utoaji wa huduma katika Sekta za Wizara Pamoja na kuratibu vikao mbali mbali vya mashirikiano baina ya SMT na SMZ kwa kushirikiana na Taasisi za Wizara.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1. Kamati inashauri Wizara kupitia programu hii, kuwekwa mipango Madhubuti na kuhakikisha wanatoa vipaumbele kwa kila mwaka wa fedha vyenye kutekelezeka lakini pia vitakavyoleta tija kwa Serikali na Wizara katika ufanisi wa kazi zake.
2. Pia, Kamati inaishauri Wizara kufanya tafiti hasa katika miradi kabla ya kuanza kwake ili kuweza kuepuka hasara na gharama zinazotokea kwa kutofanywa tafiti hizo na kusababisha hasara na upotevu wa fedha za Serikali kutokana na kufeli kwa miradi hiyo.
3. Vile vile Kamati inaendelea kusisitiza kufanyiwa marekebisha Sheria zote ambazo zimeshapitwa na wakati na utekelezaji wake hauendani na hali halisi ya sasa ikiwemo sheria ya Mthamini Mkuu wa Serikali, Sheria ya Mahkama ya Ardhi na Sheria ya Mipango Miji na Vijiji ili kuweza kuondosha changamoto iliyopo hivi sasa kwa baadhi ya sheria kukwamisha mipango ya Wizara kutokana na kuwepo kwa changamoto mbalimbali katika utekelezaji.

### 3.2:1:2 PROGRAMU NDOGO YA UTAWALA NA UENDESHAJI

Programu hii inajukumu la kusimamia uendeshaji wa shughuli za kila siku za Wizara pamoja na uendelezaji wa Rasilimali Watu kwa kuandaa mipango ya kujenga uwezo wa Watumishi, kuratibu shughuli za Viongozi wa Wizara Kitaifa na Kimataifa, kutoa uelewa kwa wafanyakazi juu ya masuala ya mtambuka, kuimarisha mazingira bora ya kazi, kushughulikia haki na stahiki za Watumishi waliopo na waliomaliza muda wao wa utumishi kwa sababu mbalimbali, kuhakikisha kuwepo kwa watendaji wa kutosha na wenye sifa pamoja na kusimamia nidhamu kwa Watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

i. Kamati inaishauri Wizara kupitia program hii ya Utawala na Uendeshaji kufanya jitihada za makusudi kutatua changamoto iliyopo ya uhaba wa wafanyakazi wa fani za kitaalamu ambao bado kuna upungufu mkubwa ili kuweza kuisaidia Wizara katika kutekeleza kazi zake hasa za kitaalamu ipasavyo na kuweza kupatikana tija iliyokusudiwa kwa maendeleo ya Nchi.

### 3.2:1:3 PROGRAMU NDOGO YA URATIBU NA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA WIZARA PEMBA

Programu hii ndogo inatekelezwa na Afisi Kuu Pemba na inajukumu la kuratibu na kusimamia utawala na mipango ya kazi za Wizara zinazotekelezwa Pemba ikiwemo Programu na Miradi ya Maendeleo.

**Changamoto zinazoikabili Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Pemba**

1. Ufinyu wa bajeti ambao unapelekea kazi kutofanyika kwa ufanisi na kukwama kwa utekelezaji wa majukumu ya Taasisi ambazo zingeleta ufanisi mkubwa wa kazi.
2. Uhaba wa uingizwaji wa fedha za matumizi jambo ambalo linapelekea Ofisi Kuu Pemba kutekeleza kazi zake katika mazingira magumu.
3. Upungufu wa wafanyakazi wataalamu kama vile wapimaji ardhi, wapangaji wa miji, Maafisa wa Ardhi, Wathamini wasaidizi wapimaji, mainjinia, Afisa Sera, Afisa Sheria na Afisa Utafiti.
4. Upungufu wa nyenzo za kufanyia kazi ikiwemo samani za Afisi, usafiri, vifaa vya kuchorea, kompyuta (computer softwares) na plotter kwa ajili ya kazi za uchorji.
5. Uhaba wa maeneo mapya yakupangwa, kupimwa na kugawiwa kwa wananchi jambo ambalo linapelekea kupungua ukusanyaji mapato.
6. Uchakavu wa baadhi ya nyumba za Serikali
7. Muamko mdogo wa kulipa kodi kwa wapangaji katika nyumba za Serikali hususan wafanyakazi wa Taasisi za Serikali.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1. Kamati inashauri wizara kuongeza bajeti kwa Ofisi kuu Pemba ili iweze kutekeleza kazi zake kwa ufanisi pamoja na kununua vitendea kazi kama vile vifaa vya kupimia na magari.

(1) Kamati inaishauri Wizara kupitia Wizara ya Fedha kulishuhulikia suala la uwingizwaji mdogo wa fedha za matumizi ambazo zinaathiri utendaji kazi wa Wizara kwa Upande wa Pemba.

(2) Kamati pia inapendekeza kufanyiwa haraka suala la wafanyakazi wataalamu ili waweze kusaidia kuleta ufanisi katika kukamilisha majukumu ya wizara Pemba.

(3) Kamati inaishauri Wizara kupitia Shirika la Nyumba kuweka utaratibu mzuri wa kukarabati nyumba za Serikali ambazo zinahitaji maboresho.

(4) Kamati inasikitishwa na hali inayoendelea ya ulipaji mdogo wa kodi kwa wapangaji katika nyumba za Serikali hususan wafanyakazi wa Taasisi za Serikali, Kamati inalitaka Shirika la Nyumba kuwachukulia hatua wale wote wanaodaiwa kodi kwa kufuata sheria na taratibui zinavyoelekeza ili Shirika liweze kujiendesha na kuweza kutumia pesa hizo kukarabati na kujenga nyumba mpya kwa maendeleo ya nchi yetu.

(5) Vile vile Kamati haikufurahishwa kwa kushindwa kufikia hata robo ya mapato waliyotakiwa kukusanya Ofisi Kuu Pemba kwa kipindi cha Julai-Disemba ambapo imejuilishwa Kamati kuwa wameweza kukusanya asilimia 9% tu ya kile walichotakiwa kukusanya kutokana na baadhi ya vyanzo kutoweza kukusanya ikiwemo chanzo cha ada ya ushauri elekezi kutokana na malimbikizo ya madeni kwa baadhi ya taasisi, kutokua tayari kutumia Ofisi ya Waakala wa Majengo katika masuala ya ujenzi na kutumia taasisi binafsi.

Kamati inaisisitiza Serikali kupitia Taasisi zake kuwatumia Wakala katika masuala yote ya ujenzi ili waweze kuleta tija na ufanisi kwa Serikali yetu Pamoja na kuingiza mapato.

## 3.2:2 PROGRAMU KUU YA USIMAMIZI WA ARDHI NA MAKAAZI

Programu hii inajukumu la kuhakikisha usalama wa matumizi ya ardhi na huduma za makaazi bora kwa Wananchi na inajumuisha Programu ndogo mbili kama ifuatavyo: -

### 3.2:2:1 PROGRAMU NDOGO YA UTATUZI WA MIGOGORO YA ARDHI

**MAHKAMA YA ARDHI**

Programu hii inatekelezwa na Mahakama ya Ardhi ambapo Mahakama ya Ardhi imeanzishwa kwa Sheria namba 7 ya mwaka 1994 kama ilivyorekebishwa na Sheria namba 1 ya mwaka 2008. Shughuli za msingi za Mahakama hii ni kupokea, kusikiliza na kuzitolea maamuzi kesi zinazotokona na migogoro ya ardhi zinazowasilishwa na wananchi pamoja na Taasisi mbalimbali.

**Changamoto zinazoikabili Mahkama ya Ardhi**

1. Bajeti ndogo ambayo haikidhi haja kwa shughuli za Mahkama ya Ardhi pamoja na kiwango kidogo cha upatikanaji wa fedha ambacho husababisha kutofikiwa malengo yaliyopangwa
2. Ufinyu wa jengo la Afisi Kuu Mwanakwerekwe
3. Uhaba wa kompyupa za kufanyia kazi
4. Uhaba wa usafiri kwa Unguja na Pemba
5. Ukosefu wa posho nyeti la wafanyakazi wa Mahkama ya Ardhi
6. Uwepo wa madeni makubwa ya wazee wa Mahkama hasa kwa upande wa Pemba.
7. Kuwepo na changamoto katika sheria no 7 ya mwaka 1994 na kupelekea shida kwenye utekelezaji wake kwa baadhi ya maeneo.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1. Kamati inashauri kwa mara nyengine tena mwaka wa fedha ujao kutengwa fedha za kutosha kwa ajili ya uendeshaji wa Mahkama na kuingizwa kwa wakati ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

2. Kamati inaitaka Wizara kulichukulia hatua suala la ufinyu wa jengo la Mahkama ya Ardhi liliopo Mwanakwerekwe kwa kutafutwa eneo jengine ambalo wataweza kulitumia kwa kazi kwani walipo sasa ni finyu na kupelekea usumbufu kwa wafanyakazi na watumiaji wa jengo hilo.

3. Kamati inashauri kuangaliwa kwa jicho la huruma Mahkama hii na kupatiwa usafiri ambao umekua ni changamoto kubwa kwao kwa Unguja na Pemba.

4. Kamati inashauri Wizara kufatilia upatikanaji wa posho nyeti ambalo wanatakiwa kupatiwa wafanyakazi wa Mahkama ya ardhi kutokana na unyeti wa kazi zao ambazo zinalingana na kazi za Mahkama nyengine.
5. Kamati inaendelea kuisisitiza Wizara kulipatia ufumbuzi suala la madeni ya wazee wa Mahkama kwa kuwalipa kwa wakati kwani imekua ni kilio kikubwa na cha muda mrefu.
6. Pia, kamati inashauri kesi za ardhi kusikilizwa na kupatiwa hukumu kwa muda mfupi ili kuepusha wahusika kupita njia zisizo sahihi kutokana na kesi kukaa muda mrefu hali ambayo inaleta zaidi changamoto na kuongezeka migongano isiyo ya lazima.
7. Vile vile Kamati inaishauri Wizara kupitia Mahkama ya Ardhi na Kamisheni ya Ardhi kufanya jitihada za makusudi kuzidi kutoa elimu juu ya masuala ya ardhi kwa wananchi ili wapate uelewa na kusaidia kupunguza migogoro ya Ardhi
8. Kamati imefarajika kuona Sheria ya Mahkama ya Ardhi namba 7 ya 1994 kama ilivyo rekebishwa na sheria namba 1 ya 2008 Ardhi imeshaanza kufanyiwa kazi lakini inaendelea kushauri kufanyiwa marekebisho na kuwasilishwa kwa Kamati na Baraza katika kipindi kijacho ili kuwezesha utatuzi wa migogoro ya ardhi kuwa kwa njia rahisi na kuondoa matumizi ya utaratibu mgumu unaotumika katika sheria ya mwenendo wa madai ambao husababisha kupoteza muda mwingi na badala yake kuanzisha utaratibu mwepesi unaojitosheleza katika kuendesha mashauri ya ardhi.

### 3.2:2:2 PROGRAMU NDOGO YA UTAWALA WA ARDHI NYUMBA NA MAKAAZI

Programu hii ndogo ina jukumu la kuhakikisha usalama wa umiliki wa ardhi na uimarishaji wa huduma za makaazi kupitia upimaji wa ardhi, utambuzi na usajili wa ardhi, mipango ya miji na matumizi ya ardhi, ukarabati wa nyumba za maendeleo na majengo ya Serikali. Programu hii ndogo inatekelezwa na Taasisi zifuatazo: -

## I. KAMISHENI YA ARDHI

Kamisheni ya Ardhi imeanzishwa kwa Sheria Namba 6 ya Mwaka 2015. Lengo la kuanzishwa kwake ni kuleta ufanisi zaidi katika kusimamia Sheria za Sekta ya Ardhi pamoja na kuziunganisha Idara zote zinazosimamia matumizi na maendeleo ya ardhi.

**Changamoto zinazoikabili Kamisheni ya Ardhi**

1) Ufinyu wa Bajeti
2) Uhaba na uchakavu wa vyombo vya usafiri
3) Uhaba wa vifaa na wataalamu kwa sekta ya Ardhi
4) Kiwango kidogo cha uelewa wa jamii juu ya dhana ya utawala na usimamizi wa ardhi.
5) Kuwepo na ardhi kubwa ambayo bado haijafanyiwa utambuzi na kusajiliwa kulingana na malengo ya usajili.
6) Kutokamilika kwa muundo wa Kamisheni ambao umekua ni wa muda mrefu.
7) Mazingira hatarishi ya jengo la Kamisheni Unguja na Pemba

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1. Kamati inashauri Kamisheni ya Ardhi kufanya mashirikiano na Taasisi mbalimbali katika kutunza na kuendeleza masuala ya ardhi ikiwemo Mahkama ya Ardhi, ZAWA, Mamlaka ya Serikali za Mitaa pamoja na wahusika wa Mipango Miji na Vijiji.
2. Kamati inashauri Kamisheni kuzidi kutoa elimu kwa umma juu ya masuala yote ya Ardhi ili kuepusha migogoro isiyo ya lazima katika jamii.
3. Kamati pia inashauri Kamisheni kupitia Wizara kufanya marekebisho ya sheria zao ambazo zinakwaza katika utekelezaji wa majukumu yao.
4. Aidha, kamati inashauri Wizara kuliangalia suala zima la changamoto kubwa ya usafiri kwa afisi zake za Unguja na Pemba.

5. Kamati inasisitiza kuchukuliwa hatua za haraka suala la uvamizi wa ardhi za Serikali, kilimo na eka 3 ili kuepusha athari za kimazingira pamoja na upotevu wa ardhi kiholela usiozingatia sheria na taratibu zilizowekwa.
6. Pia, kamati inaendelea kupendekeza kupitia Wizara kuangalia utaratibu mzuri wa upimaji maeneo ambayo yameshalipiwa kwa kuangalia njia ambayo wataweza kuzipata fedha zilizokwisha kulipwa ambazo zinatakiwa kutumika katika kazi ya kupima maeneo hayo.
7. Vile vile kamati inashauri kuangaliwa suala la majengo la Kamisheni kwa Unguja na Pemba na kuchukuliwa hatua zinazofaa.
8. Kamati inatoa wito kwa Wizara kupitia Kamisheni kuhakikisha wananchi wote waliolipa kupimiwa wanapimiwa ili kuondosha malalamiko yaliopo kwa wananchi kutokana na kuchukua muda mrefu bila kupata huduma hii.

## II. OFISI YA MTHAMINI MKUU WA SERIKALI

Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali imeanzishwa kwa Sheria Namba 5 ya mwaka 2015 kwa dhumuni la kuhakikisha usimamizi mzuri wa kazi za uthamini kwa Serikali, Sekta binafsi na wananchi kwa ujumla. Kazi kuu ya Mthamini Mkuu ni kuthibitisha kazi za uthamini zinazofanywa nchini na wathamini wa Taasisi za Serikali na Kampuni binafsi.

**Changamoto zinazoikabili Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali**

1. Ufinyu na upatikanaji wa fedha za bajeti kwa matumizi ya kazi za kawaida.
2. Uhaba wa samani na vitendea kazi vya Ofisini na uwandani (field)
3. Uhaba wa vyombo vya usafiri hasa vyombo vya maringi mawili
4. Kukosekana kwa mfumo wa kisasa (kidigitali) wa kuhifadhia ripoti za uthamini.
5. Ukosefu wa eneo la Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali Pemba
6. Uhaba wa wafanyakazi wenye taaluma ya uthamini wa mali.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1. Kamati inashauri Serikali kupitia wizara katika mwaka wa fedha ujao kuwapatia bajeti itakayowasaidia kutekeleza kazi walizojipangia na kupatiwa kwa wakati.

2. Kamati inaisisitiza Wizara kuwapatia samani na vitendea kazi Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali ili waweze kufanikisha majukumu yao ipasavyo.

3. Kamati inaishauri Wizara kuiangalia Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali kwa kuwapatia usafiri ambao utawawezesha kukamilisha kazi zao kwa ufanisi, kwani kwa hivi sasa imejuilishwa Kamati kuwa wanatumia vyombo vyao binafsi kwa ajili ya kutekeleza kazi zao.

4. Kamati pia inasisitiza kukamilishwa mfumo wa kieletroniki utakaotumika kuingiza taarifa za mali zilizofanyiwa uthamini ili kuwe na rikodi rasmi ambayo itasaidia kuhifadhi taarifa zote za kazi zinazofanywa na Ofisi ya Mthamini Mkuu lakini pia kusaidia kuwepo kwa taarifa ambazo kwa sasa zinakosekana, ambapo kwa sasa wameijuilisha Kamati kuwa bado wanatumia mfumo wa excel kutunza taarifa za uthamini.

5. Kamati imesikitishwa na taarifa ya kukosekana kwa eneo la Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali Pemba na inaishauri Wizara kuchukua jitihada za makusudi ili kutatua changamoto hii kwani imekua ikiviza ufanisi wa kazi za Uthamini.

6. Pia, Kamati inaona ni busara kufanya jitihada za haraka za kupatikana wafanyakazi wenye taaluma ya uthamini wa mali ili waweze kuisaidia Wizara katika kufanikisha malengo yao.

7. Kamati inaishauri Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali kupitia wataalamu kutumia taaluma zao vizuri na kuishauri Serikali.

8. Kamati vile vile, inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Fedha kuwapatia Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali gawiyo la angalau 40% linatokanalo na makusanyo yao ili waweze kutekeleza kazi zao kwa wakati na kununua vifaa vya kisasa vya uthamini ili kuimarisha usimamizi mzuri wa kazi za uthamini kwa wadau mbalimbali.

## III. WAKALA WA MAJENGO ZANZIBAR (ZBA)

Wakala wa Majengo imeanzishwa kwa Tangazo la Kisheria (Legal Notice) namba 50 ya mwaka 2017. Lengo la kuanzishwa Wakala wa Majengo ni kutoa huduma ya Makaazi kwa Viongozi Wakuu, Maafisa Wakuu Waandamizi wa Serikali na Watumishi wa Umma. Aidha, Wakala wa Majengo ina wajibu wa kusimamia na kuratibu miradi ya ujenzi na matengenezo ya majengo ya Serikali ili kuhakikisha ubora wa majengo hayo.

**CHANGAMOTO ZINAZOKABILI WAKALA WA MAJENGO**

1. Ukosefu wa fedha za kutekelezea majukumu waliojipangia
2. Ukosefu wa Ofisi ya kudumu. Bado Wakala wa Majengo hawana ofisi za kudumu hali ambayo inawaletea usumbufu kwani wamekua wakiazimwa na baada ya muda wanalazimika kuhama.
3. Wakala kukabidhiwa nyumba za Serikali ambazo ni chakavu zinazohitaji matengenezo makubwa
4. Upungufu wa vitendea kazi pamoja na teknolojia za kisasa
5. Baadhi ya Miradi ya Serikali bado haipitii kwa Wakala wa Serikali
6. Kuwepo na uelewa mdogo kwa baadhi ya Taasisi za Serikali juu ya majukumu ya Wakala wa Majengo katika usiamamizi wa nyumba za Serikali.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1. Kamati inashauri Serikali kupitia Wizara ya Fedha kuwaangalia Wakala kwa mwaka wa fedha ujao kwa kuwapatia fedha ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo.
2. Pia, Kamati inashauri kuwe na utaratibu mzuri wa uingizwaji wa fedha zinazopangwa ili waweze kuzitumia kwa kukamilisha malengo yao ikiwemo la kukarabati nyumba za Serikali ambazo nyingi ni chakavu.
3. Pia, kamati inaisisitiza wizara kuchukua jitihada za makusudi kulifanyia kazi suala la kuwapatia Afisi Wakala wa Majengo ili waweze kuondokana na usumbufu walionao kwa sasa.
4. Vile vile, kutokana na umuhimu wa Taasisi hii kamati inaona ni vyema wakapatiwa vitendea kazi ambavyo vitawawezesha kufanikisha majukumu yao ipasavyo.

5. Kamati inatoa wito kwa Serikali kuwatumia Wakala wa Majengo katika miradi yao ili waweze kutoa ushauri wa kitaalamu na kuweza kusaidia kufanikiwa kwa miradi hiyo na kwa na ubora unaotakiwa.
6. Kamati pia, inashauri kutolewa elimu kwa Taasisi zote za Serikali juu ya umuhimu wa kuwepo Taasisi hii na majukumu yake ili ziweze kusaidia kufanikisha lengo lililokusudiwa.
7. Kamati inaitaka wizara kuchukua hatua za makusudi kupatikana wafanyakazi wataalamu wenye upungufu katika Taasisi hii ambao ni muhimu kuweza kufanikisha utendaji kazi za ofisi.

## IV. SHIRIKA LA NYUMBA ZANZIBAR

Shirika la Nyumba Zanzibar (ZHC) limeanzishwa kwa Sheria namba 6 ya mwaka 2014. Lengo la kuanzishwa Taasisi hii ni kuwawezesha Wananchi kupata makaazi bora na salama pamoja na kuziimarisha nyumba za Shirika zilizopo na kujenga nyumba mpya. Kamati imebahatika kutembelea Shirika la Nyumba pamoja na kukagua nyumba mbali mbali zinazomilikiwa na Shirika. Pia imeweza kutembea Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) na kujifunza mambo mbali mbali.

### Changamoto zinazokabili Shirika la Nyumba

1. Kuwepo kwa madeni makubwa na ya muda mrefu kwa wapangaji wa shirika jambo ambalo linasababisha kukosekana fedha na kucheleweshwa kwa utekelezaji wa mipango ya Shirika ya ujenzi wa nyumba mpya na matengenezo ya nyumba zilizopo.
2. Kuwepo kwa madai ya baadhi ya viongozi kutolipa kodi na kuwakingia vifua wapangaji wengine na kukwamisha juhudi za Shirika za kufikia lengo lilokusudiwa.
3. Uchakavu wa nyumba za Shirika (Nyumba za Maendeleo, Mji Mkongwe na Vijijini) kutokana na kukaa muda mrefu bila kufanyiwa matengenezo
4. Shirika kutokidhi mahitaji ya nyumba na makaazi kwa Zanzibar, kwani mahitaji ya nyumba ni makubwa mno na uwezo wa Shirika wa kukidhi mahitaji hayoi ni mdogo.
5. Kodi za nyumba ni ndogo ukilinganisha na gharama za matengenezo ya nyumba hizo inapelekea Shirika kushindwa kufanya matengenezo kwa kiwango kinachotakiwa.
6. Kuwepo na riba kubwa kutoka taasisi za kifedha ikiwemo mabenki ambapo Shirika linashindwa kukopa fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba mpya.

7. Utunzaji mbovu wa nyumba za Serikali kwa wapangaji wanaoishi katika nyumba za Shirika.
8. Ukosefu wa hatimiliki kwa nyumba za Shirika.
9. Uhaba wa fedha za kufanyia matengenezo nyumba ambazo baadhi yake ni mbovu sana na zinahitaji fedha nyingi kufanyiwa marekebisho.
10. Upungufu wa wataalamu wa fani za ujenzi.
11. Uhaba wa usafiri kwa ajili ya kufatilia shughuli za Ofisi
12. Matumizi yasiyo sahii ya nyumba za Shirika.
13. Mazingira machafu katika maeneo ya nyumba za shirika.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1) Kamati inaendelea kuwashauri Shirika kuchukua hatua na mbinu mbadala katika kuhakikisha wale wote wanaodaiwa kulipa kwa kufata utaratibu ili Shirika liweze kuinuka na kutekeleza kazi zake ikiwemo ukarabati wa nyumba. Lakini pia kamati inalitaka shirika kuchukua jitihada mbadala kuhakikisha deni kutoongezeka.
2) Kamati pia inaitaka wizara kuliangalia na kulichukulia hatua zinazofaa suala la nyumba zisizofaa kimatumizi ili kuepusha athari kwa wakaaji na Serikali kwa ujumla.
3) Kamati haikufurahishwa na suala la ukosefu wa hatimili za nyumba za Shirika hivyo, inaitaka wizara kuchukua jitihada za ziada kuweza kuzipatia nyumba zote za Shirika hatimili kwani limekua ni tatizo la muda mrefu sasa.
4) Kamati inashauri pia kuchukuliwa hatua za upatikanaji wa wataalamu za fani za ujenzi ambao watakaosaidia kuweza kushauri na kufanikisha majukumu ya Shirika.
5) Kamati imesikitishwa na uwepo wa matumizi mabaya ya nyumba yanayofanywa na wapangaji hao ambayo yameharibu na kuleta hasara kwa Shirika, hivyo kamati kwa mara nyengine tena inalita Shirika kuandaa muongozo maalum utakaoonesha utaratibu mzima wa ukaaji katika nyumba hizo na kwa atakaeshindwa kuweza kuchukuliwa hatua ikiwemo kuondoshwa katika nyumba izo, lengo kuweza kuondosha tabia ya uharifu unaofanywa na wakaazi wa nyumba hizo ambao umeshaathiri nyumba na kuipa hasara Serikali.
6) Kamati inashauri katika bajeti ijayo kuangaliwa suala la usafiri ambalo ni muhimu sana katika ufatiliaji wa majukumu ya Shirika ya kila siku.
7) Vile vile kamati kwa mara nyengine tena inalisisitiza Shirika kushirikiana na Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Halmashauri na

Masheha kuhakikisha suala la usafi katika mazingira ya nyumba za Shirika linapewa kipaumbele.

8) Kamati inaendelea kusisitiza Uhakiki wa wapangaji uwe endelevu ili kuweza kuwatambua wapangaji wote pamoja na kuhakikisha wateja wao wote kuwa na mikataba.
9) Vile vile Kamati inaishauri Wizara kuangalia njia mbadala ya kutafuta benki zenye unafuu wa riba na kuweza kukopa ili waweze kufanikisha ujenzi wa nyumba mpya pamoja na kufanikisha malengo yao bila kukwazika.

10) Vile vile Kamati katika kutekeleza majukumu yake imeweza pia kukutana na kupokea taarifa ya Bodi ya Kondominio, Bodi ya Usajili Wasanifu Wahandisi na Wakadiriaji Majengo na Bodi ya Usajili wa Wakandarasi Zanzibar (zcrb) na kuweza kupata yafuatayo: -

### A. BODI YA KONDOMINIO

Bodi hii imeanzishwa kwa Sheria ya Kondominio namba 10 ya mwaka 2010. Lengo la kuanzishwa Bodi ya Kondominio ni kusajili, kuratibu na kusimamia matumizi ya pamoja kwa majengo yenye sehemu zinazomilikiwa na watu tofauti,kusuluhisha migogoro ya makaazi katika majengo na kufatilia na kusimamia ukarabati wa majengo yanayojumuisha wamiliki wengi.

**Changamoto za Bodi ya Kondominio**

1. Kuwepo kwa miradi hususan ya Serikali ambayo haijkamilisha taratibu za usajili
2. Ukosefu wa watendaji wa kada za kitaalamu kwa ajili ya kurahisisha kazi ya usajili ikiwemo mkadiriaji majengo (QS),real estate,na mtunza kumbukumbu.
3. Uchakavu wa sehemu ya juu ya jengo la Kondominio ambalo linasababisha uhaba wa nafasi katika jengo la Afisi ya Bodi.
4. Kamati imejuilishwa kuwepo na changamoto ya kutokamilika kwa vielelezo vya umiliki wa waombaji.
5. Kuwepo kwa maombi mengi ambayo yanahitaji kupatikana ithibati ya mirathi
6. Kuchelewa kupatikana kwa maoni ya Afisi ya Wilaya yanayohusiana na maombi ya usajili
7. Kuwepo kwa miradi ambayo haifuati taratibu za usajili wa Kondominio kupitia Sheria ya Kondominio.

8. Ukosefu wa usafiri, Upungufu wa wataalamu na Kukosekana kwa usimamizi mzuri wa nyumba za maendeleo.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1. Kamati inaihimiza Wizara kupitia Bodi kuhakikisha miradi yote ya Serikali inasajiliwa kama utaratibu unavyoelekeza ili kuweza kufikiwa malengo yaliyokusudiwa
2. Pia, Kamati inasisitiza kuchukuliwa jitihada za makusudi kupatikana watendaji wanaohitajika wa kada za kitaalamu ili kuwezaa kurahisha kazi za usajili.
3. Kwa mara nyengine tena Kamati inaishauri wizara kushughulikia suala la kulifanyia matengenezo jengo linalotumiwa na bodi ili waweze kuwa na sehemu zakutosha kufanyia kazi kwa kuwatengea bajeti maalum ya kukarabati jengo.
4. Kamati inashauri kutolewa elimu ya kutosha juu ya umuhimu na taratibu za usaji wa Kondominio ili kuepusha changamoto ya mapungufu kwa baadhi ya vielelezo vwa waombaji ambavyo vinapelekea kukwamisha kukamilika kwa usajili na kuleta usumbufu.
5. Kamati inaishauri Bodi kufanya jitihada za makusudi kwa kushirikiana na Afisi ya Wakfu na Mali ya Amana kuweza kurahisha upatikanaji wa ithibati ya mirathi pale inapohitajika.
6. Pia, Kamati inaishauri Bodi kuwa na mashirikiano mazuri na Afisi ya Wilaya ili kuweza kupatikana maoni yao kwa muda muwafaka na kurahisisha zoezi la maombi ya usajili.
7. Kamati inashauri kuwepo na utaratibu wa kuchukuliwa hatua kwa miradi yote isiyofuata taratibu za usajili wa Kondominio kama sheria inavyoelekeza.
8. Kamati inaendelea kuishauri Wizara kuwapatia usafiri wa uhakika pamoja na kuwepo usimamizi mzuri wa nyumba za maendeleo ambao utaiwezesha bodi kufanya majukumu yake kwa ufanisi.

**B. BODI YA USAJILI WASANIFU WAHANDISI NA WAKADIRIAJI MAJENGO**

Bodi hii imeanzishwa kwa Sheria ya Usajili wa Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo namba 5 ya Mwaka 2008. Lengo la kuanzishwa kwa Bodi hii ni kusimamia, kudhibiti na kuwaendeleza wataalamu wa ujenzi ili wafanye kazi zao kwa utaalamu na viwango vinavyotakiwa.

**Changamoto za Bodi ya Usajili Wasanifu Wahandisi na Wakadiriaji Majengo**

1. Bodi kushindwa kutekeleza majukumu yake kutokana na ukosefu wa fedha kama ilivyoainishwa katika bajeti.
2. Ukosefu wa watendaji wa kudumu unaopelekea kupungua kazi ya utendaji.
3. Kutojisajili kwa baadhi ya wataalamu wa kigeni hasa wale wanaofanya kazi katika miradi ya maendeleo inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo ambalo ni kosa kwa mujibu wa sheria.
4. Wataalamu waliosajiliwa kuchelewa kulipa ada ya mwaka.
5. Bodi kushindwa kuwaendeleza wahitimu waliosajiliwa na bodi kutokana na ukosefu wa fedha.
6. Ukosefu wa jengo la ofisi za kudumu kwa Bodi.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMAMATI**

1) Kamati inataka Wizara kulichukulia hatua suala zima la upatikanaji wa fedha za bajeti kwa mwaka wa fedha ujao ili Bodi iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.
2) Pia, Kamati inaitaka Wizara kupitia Idara ya Uendeshaji na Utumishi kuwa na mipango Madhubuti na kuhakikisha Bodi inapata watendaji wa kudumu ambao wataweza kuisaidia kufanikisha kazi zake.
3) Kamati inashauri kuwekwa utaratibu maalum utakaowataka wataalamu wa kigeni kujisajili na kuchukuliwa hatua kama ambavyo sheria inaelekeza.
4) Vilevile Kamati inaitaka Bodi kupitia Wizara kuwa na njia Madhubuti na kuweza kuwachukulia hatua ikiwemo yakulipa faini wale ambao watachelewa kulipa ada ya mwaka.
5) Kamati inaitaka Wizara kuweka mpango maalum katika bajeti yao kwa ajili ya kuwaendeleza wahitimu waliosajiliwa na Bodi ili kuwepo na ufanisi wakutosha kupitia fani zao na kuweza kuisaidia Bodi kutekeleza majukumu yake.

**C. BODI YA USAJILI WA WAKANDARASI ZANZIBAR (ZCRB)**

Bodi ya Usajili wa Wakandarasi imeanzishwa kwa sheria namba 6 ya mwaka 2008, lengo la kundwaa kwake ni kusimamia wakandarasi wote wanaofanya kazi Zanzibar na kuhakikisha wanajenga kwa kufuata kanuni na taratibu zote zikiwemo za usalama katika maeneo ya ujenzi. Pia jukumu la msingi la bodi hii ni kuwasajili na kuwasimamia Wakandarasi wa Ujenzi na kuwaendeleza kitaalamu kwa kuwapa mafunzo mafupi Pamoja na kusajili miradi yao.

**Changamoto za Bodi ya Wakandarasi**

1. Ukosefu wa jengo la kudumu la Afisi hali inayopelekea kukosekana kwa utulivu katika kutekeleza kazi zake.
2. Kukosekana kwa ushirikiano kwa baadhi ya Taasisi za Serikali katika kusajili miradi yao.
3. Kukosekana kwa muundo wa Bodi.
4. Uhaba wa nyenzo za kufanyia kazi jambo ambalo linapelekea Bodi kushindwa kufanya ukaguzi na kupunguza mapato kwa Serikali.
5. Uwepo wa baadhi ya Taasisi za Serikali kufanya miradi kama wakandarasi bila kusajiliwa na Bodi.
6. Kukosekana kwa gawiyo katika makusanyo ya Bodi hali ambayo inapelekea bodi kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa wakati kutokana na fedha za Bodi kutopatikana kama inavyohitajika.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1. Kamati inaishauri Wizara kuchukua jitihada za makusudi kuhakikisha Bodi inapata jengo la kudumu kwa mwaka wa fedha ujao ili waweze kutekeleza kazi zao kwa ufanisi.
2. Kamati inaishauri Wizara kupitia bodi kukaa pamoja na Taasisi zote ambazo hazitoi ushirikiano wakati wa kusajili miradi yao na kumaliza changamoto hiyo.
3. Vile vile kamati inasikitika kukosena kwa Muundo wa Bodi na inasisitiza kuchukuliwa hatua ili kukamilishwa muundo huo.
4. Kamati pia inaitaka wizara kuchukua hatua za makusudi kuhakikisha suala la ukosefu wa nyenzo za kufanyia kazi linapatiwa ufumbuzi kwa mwaka huu wa fedha.
5. Kamati haikufurahishwa na tabia ya baadhi ya Taasisi za Serikali zinazofanya miradi kama wakandarasi bila kusajiliwa na bodi, hivyo, Kamati inaitaka Wizara kufatilia Taasisi zote zinazofanya makosa hayo na kuzichukulia hatua.

6. Pia kamati inaishauri Wizara kupitia Wizara ya fedha kuwapatia Bodi gawiyo la makusanyo yao kama sehemu itakayowasaidia kuweza kufanikisha kazi zao.

## WIZARA YA MAJI NISHATI NA MADINI

## 4.0 MAJUKUMU NA MUUNDO WA WIZARA

Wizara ya Maji, Nishati na Madini ni miongoni mwa Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye lengo la kuhakikisha wananchi wote wanapata maji safi na salama, huduma ya nishati ya umeme na rasilimali zisizorejesheka bila ya usumbufu Mjini na Vijijini.

Wizara hii inaundwa na Idara nne na Taasisi tatu. Idara na taasisi hizo ni: -

i. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti,

ii. Idara ya Nishati na Madini,

iii. Idara ya Utumishi na Uendashaji,

iv. Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba,

v. Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA),

vi. Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO)

vii. Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (ZURA).

## 4.2 PROGRAMU ZA WIZARA

Kwa kipindi hiki Wizara hii inaendelea na utekelezaji wa Programu zake Kuu ambazo ni; -

1) Programu ya Usimamizi wa Huduma za Maji
2) Programu ya Usimamizi wa Huduma za Nishati na Madini
3) Prograamu ya Uendeshaji na Uratibu wa Mipango ya Wizara

## 4.3 PROGRAMU YA USIMAMIZI WA HUDUMA ZA MAJI

Kamati ilipata fursa ya kupokea taarifa za Utekelezaji pamoja na kutembelea baadhi ya maeneo ya utekelezaji wa programu hii ambayo

inatekelezwa na Idara ya Maji pamoja na Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA).

**4.3:1 IDARA YA MAENDELEO YA MAJI**

1. Idara ya Maendeleo ya Maji ina jukumu la kusimamia masuala yanayohusu Sekta ya Maji nchini. Kamati ilifanya mahojiano na wakuu wa Idara hiyo na kubaini yafuatayo:-

2. Idara imefanikiwa kufanya tathmini ya awali ya kuyatambua na kuyaanisha maeneo yote yanayatarajiwa kuanzishwa mfumo jumuishi wa ukusanyaji taarifa za rasilimali maji katika vyanzo vya maji vilivyopo Unguja na Pemba.

3. Kuandaa rasimu ya Mpango Mkakati wa Mahitaji ya Maji Zanzibar.

4. Idara inaendelea kufuatilia kwa karibu Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar (EXIM INDIA).

5. Idara ya Maendeleo ya Maji imekamilisha hatua za utayarishaji wa hadidu rejea kwa ajili ya kumtafuta mtaalamu atakayefanya kazi ya utayarishaji wa Upembuzi Yakinifu kuhusiana na uibuaji wa vyanzo mbadala vya maji.

**4.3:2 CHANGAMOTO ZA IDARA YA MAENDELEO YA MAJI**

1. Kukosekana kwa baadhi ya wataalamu wa sekta ya maji katika fani ya Miamba ya Maji (Hydrogeologist).
2. Kutokuwepo Kwa mfumo wa usimamizi na ukaguzi wa vyanzo vya maji.
3. Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar (EXIM INDIA) kutotekelezwa kwa haraka na kwa muda uliopangwa kutokana kuchelewa kwa utoaji wa vifaa bandarini.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1. Kamati inaiagiza Idara ya Maendeleo ya Maji kuandaa na kuwasilisha mahitaji ya rasilimali watu ya Idara hiyo kwa Uongozi wa Wizara kwa ajili ya kupatiwa wataalamu katika fani husika.

2. Idara ianzishe Mfumo Jumuishi wa Usimamizi wa Rasilimali Maji (Integrated Water Monitoring System) katika vyanzo vya maji.

### 4.3:5 MAMLAKA YA MAJI ZANZIBAR (ZAWA)

Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) pamoja na mambo mengine ina jukumu la kuzalisha na kusambaza huduma ya Maji safi na salama kwa wananchi wote Zanzibar mjini na Vijijini kwa uhakika.

**Hali halisi ya upatikanaji wa maji Zanzibar**

Kamati imebaini kuwa hadi kufikia Disemba 2022, uzalishaji wa maji umefikia wastani wa asilimia **66%** kwa Unguja na Pemba ambapo mahitaji ni lita **241,769,168** kwa siku, na uzalishaji kwa siku ni lita **51,087,187** hali inayopelekea mapungufu kwa siku kuwa ni lita **103,863,093.** Kamati imegundua asilimia hiyo inatokana na uzalishaji wa Visima **303** vinavyomilikiwa na ZAWA ambapo kati hivyo, visima **53** havitoi huduma kutokana na hitilafu mbali mbali.

**Miradi ya Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji wa Maji (EXIM Bank 92.18 USD) na Programu ya Ahueni ya UVIKO-19**

Kamati imearifiwa kwamba kukamilika kwa Miradi ya Uhuishaji na Uimarishaji wa mfumo wa usambazaji wa maji (EXIM Bank 92.18 USD) na Programu ya Ahueni ya UVIKO-19 kutaongeza visima vipya 102, matangi 25 makubwa ya kuhifadhia maji pamoja na kuimarisha mtandao wa maji kwa masafa ya kilomita 792 kwa Unguja na Pemba. Kukamilika kwa miradi hiyo, uzalishaji wa maji utafikia lita **356,117,075** kwa siku kiwango ambacho kitafikisha zaidi ya asilimia **100%** hapa Zanzibar. ZAWA inadai kuwa hatua hiyo itapunguza tatizo la maji kwa asilimia kubwa.

### 4.3:6 CHANGAMOTO ZA ZAWA

Baada ya kupokea taarifa za ZAWA pamoja na kuhojiana naWafanyakazi na kutembelea Miradi wanayoisimamia, Kamati imegundua kwamba ZAWA inakabiliwa na Changamoto kadhaa katika kutekeleza majukumu yake ikiwemo zifuatazo: -

a) Uhaba wa wataalamu katika fani za Uhandisi.

b) Kupanda na kushuka kwa umeme mara kwa mara kunakopelekea hitilafu za kuungua pampu na vifaa katika visima.
c) Muitikio mdogo wa Wananchi wengi katika kulipia huduma ya maji.
d) Uchakavu wa Miundombinu ya maji hususan bomba za Asbestos cement (AC) na uPVC.
e) Kukosekana kwa hatimiliki katika maeneo ya vianzio vya maji.
f) Uvamizi wa maeneo ya vianzio vya maji pamoja hujuma za miundombinu ya maji.
g) Malalamiko ya limbikizo la tofauti ya mshahara mpya kwa wafanyakazi tangu mwaka 2017.
h) Ongezeko kubwa la vianzio na Miundombinu ya maji linalopelekea Mamlaka ya Maji kuhitaji wafanyakazi wengi kusimamia.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1) Kamati inaiagiza ZAWA kuomba wataalamu kupitia OR- Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, ili kuweza kukidhi mahitaji na kuleta ufanisi katika utendaji wa kazi za Mamlaka.

2) Kamati inaishauri ZAWA na Serikali kwa ujumla Kufanya maboresho ya miundominu ya maji kwa kubadilisha bomba chakavu na kulaza mpya, ili kuweza kuhuwisha huduma ya maji na kuwa endelevu katika maeneo yote ya Mjini na Vijijini.

3) Kwa mara nyengine tena, Kamati inaishauri ZAWA kuyahifadhi maeneo ya vianzio vya maji pamoja na miundombinu kwa kujenga uzio, kutafuta hatimiliki na kuweka ulinzi ili kuepusha uvamizi na uharibifu katika maeneo hayo.

4) Kamati inaishauri ZAWA kushirikiana na ZECO na wahakikishe wanafunga vifaa maalum vya kudhibiti ongezeko la umeme, ili kuepusha uunguaji wa Pampu na vifaa mara kwa mara

5) Mamlaka ifuatilie kwa karibu zaidi suala la madai ya malimbikizo ya tofauti ya mishahara ya wafanyakazi OR-Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwani limekuwa la muda mrefu na kuwakatisha tamaa wafanyakazi wa ZAWA.

6) Kamati inaisisitiza ZAWA kufuatilia na kuhakikisha Miradi ya Mipya inamalizika kwa wakati uliopangwa pamoja na kusawazisha miradi ya zamani ili kuondosha tatizo la maji na kwenda sambamba na malengo ya

Serikali ya Awamu wa Nane.

## 4.4 PROGRAMU YA USIMAMIZI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MADINI

### 4.4:1 IDARA YA NISHATI NA MADINI

Idara ya Nishati na Madini ina jukumu la kusimamia masuala yote yanayohusiana na Nishati na Madini ikiwemo Maliasili Zisizorejesheka pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa maliasili hizo. Katika mahojiano na Idara hii, Kamati imebaini kwamba;-

a) Azma ya kuhakikishan kuwa Zanzibar inakuwa na chanzo chake cha kuzalisha umeme ipo katika hatua za mwisho za majadiliano na Mwekezaji.

b) Idara bado ipo katika hatua za mwisho kukamilisha mpango mkuu wa miaka 30 wa matumizi ya nishati ya Umeme.

c) Idara imetayarisha andiko la miradi (concept note) itakayoweza kuisaidia Serikali kutatua changamoto za nishati Zanzibar.

### 4.4:2 SHIRIKA LA UMEME ZANZIBAR (ZECO)

Shirika la Umeme Zanzibar linajukumu la kusimamia upatikanaji wa huduma ya umeme kwa wananchi wote wa Zanzibar. Kamati imebaini kwamba kwa kipindi hiki ZECO imeendelea kuimarisha Miundombinu ya Umeme, ili wananchi waweze kupata huduma ya umeme kwa uhakika kwa Kubadilisha nguzo mbovu, Kusawazisha maeneo yenye umeme mdogo, Ukaguzi wa Transfoma na Uunganishaji wa wateja wapya.

### 4.4:3 Changamoto za ZECO

Kamati imebeini kwamba bado ZECO inakabiliwa na changamoto kubwa ambazo zimekuwa zikiripotiwa katika ripoti nyingi za kamati hii zilizopita. Miongoni mwa Changamoto hizo ni:-

1. Uwepo wa madeni makubwa kwa Taasisi za SMZ, SMT na Taasisi Binafsi hadi kufikia Shilingi **56,745,448,111.52** (hadi kufikia Disemba 22).

2. Kuwepo na umeme mdogo ambao katika maeneo mengi .

3. Ukatikaji wa mara kwa mara wa huduma ya Umeme katika maeneo mengi ya Zanzibar.

4. Utaratibu usioepukika wa matumizi ya kabla ya malipo kwa baadhi ya Taasisi.

5. Kutokufanikiwa juhudi za kudai madeni kwa baadhi taasisi za Serikali.

6. Uchache wa wafanyakazi na vifaa kulingana na ongezeko kubwa la wateja wapya wanaohitaji kuungiwa umeme.

7. Uhaba wa vitendea kazi, ikiwemo vifaa vya kazi na usafiri.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1. Kwa mara nyengine tena, Kamati inashauri Shirika kuzidi kujipanga katika kuboresha upatikanaji wa huduma ya nishati ya umeme ambapo mahitaji yanaongezeka siku hadi siku.

2. Kamati inaihimiza ZECO kwa kushirikiana na Wizara kuendelea kufatilia wadaiwa wote wa Taasisi za Serikali ili kusawazisha madeni yao na kuliwezesha shirika kutoa huduma bora zaidi.

3. Kamati inaendelea kuishauri ZECO kuzidisha ulinzi na kuihifadhi miundombinu yake yote ili kujiepusha na uharibifu unaoweza kujitokeza.

4. Kamati inaishauri Wizara kulipatia ufumbuzi suala la uhaba wa vitendea kazi ikiwemo usafiri ili waweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.
5. Kamati imegundua changamoto kadhaa zilizoibuliwa katika ukaguzi uliofanywa na ZURA, Kamati inashauri kuchukua hatua za haraka kusawazisha kasoro hizo.

**4.4:4 MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI ZANZIBAR (ZURA)**

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar – ZURA ina jukumu la kudhibiti huduma za maji na nishati Zanzibar, ili kuhakikisha huduma hizo zinapatikana kwa kiwango bora.

### 4.4:4 UKAGUZI WA ZURA

### 4.4:5:1 Ukaguzi wa ZURA katika miundombinu ya ZAWA

a) Maeneo mengi yaliyokaguliwa yalionesha kukidhi viwango vya ubora wa matumizi ya binadamu katika nyanja ya (physiochemical parameter).
b) Maeneo machache yamegundulika kuwa na kiwango kikubwa cha chumvi kinachokaribia kuvuka kiwango cha ubora wa matumizi.

c) Baadhi ya mitambo inayotumika kutibu maji kabla ya kusambazwa kwa watumiaji (*Water treatment facilities)* haifanyi kazi.

### 4.4:5:2 Ukaguzi wa ZURA katika miundombinu ya ZECO

Kwa pipindi cha Julai – Disemba 2022 ZURA ilikagua ZECO na ukaguzi huo ulibaini yafuatayo;-

*a)* Transfoma 11 zimeungwa moja kwa moja katika njia za kusambazia umeme kwa wananchi bila ya kutumia kifaa cha kudhibiti umeme (fuse).
b) Transforma nane (8) zimeungwa moja kwa moja kwa kutumia waya katika sehemu ya kupokelea umeme mkubwa.
c) Transfoma nyingi zilizokaguliwa zilikutwa zimezongwa na miti**.**

### MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

1. ZURA ihakikishe inaziandikia taasisi za ZAWA na ZECO na kurejesha mrejesho wa yale yote yanayoibuliwa wakati Mamlaka hiyo inapofanya Ukaguzi kwa taasisi inazozisimamia.

## 4.5 SEKTA YA MADINI

### 4.5:1 Rasilimali ya Mchanga na Kifusi

Kamati imebaini kwamba Idara ya Nishati na Madini imeanza kupeleka mfumo wa kielektroniki katika ngazi za Wilaya ili kukabili utumiaji wa mfumo wa Usimamizi wa Madini kwa wananchi, ili kuondoa mrundikano wa maombi na ambapo kwa sasa, mwananchi atapatiwa kibali cha madini ya ujenzi ndani ya masaa nane (8) badala ya siku mbili za hapo awali.

### 4.5:2 Magari ya Mchanga Taveta

Kamati ilitembelea Magari ya Mchanga Taveta, Wilaya ya Magharibi B na kulikagua eneo hilo pamoja na kufanya mahojiano na Vijana wanaojishughulisha na biashara ya mchanga katika eneo hilo na kubaini changamoto zifuatazo:-

a) Eneo hilo sio rafiki kiusalama na kimazingira

b) Eneo lipo chini ya Line za Umeme Mkubwa unaotokea Fumba kuelekea Mtoni

c) Shughuli zinazofanyika katika eneo hilo linaikosesha mapato serikali

### 4.5:3 Uhuishwaji wa maeneo ya uvunaji Rasilimali zisizotejesheka

Kamati ilipata fursa ya kukagua uhuishwaji wa maeneo ya uvunaji wa rasilimali zisizorejesheka za Wilaya ya Kaskazini 'B' na kushuhudia maeneo kadhaa yanayohuishwa na Serikali yakiwa katika hali isiyoridhisha huko maeneo yanayosimamiwa na watu binafsi yakinawiri vizuri na kuonesha matumaini na dalili njema za kunawiri.

### 4.5:4 Changamoto katika Sekta ya Madini

a) Kukosekana Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo katika sekta ya Madini Zanzibar.
b) Kukosekana kwa Maabara ya Jiolojia na taarifa za kijiolojia.
c) Upungufu wa wataalamu wa Madini.
d) Uchimbaji na uvunaji holela wa rasiimali zisizorejesheka
e) Gharama kubwa za uhuishaji maeneo ya uvunaji wa rasilimali zisizorejesheka

### MAAGIZO NA USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

1. Kamati inaendelea kuisisitiza Wizara kandaa Sera, Sheria na Kanuni za usimamizi wa Madini Zanzibar ili kupata miongozo bora ya kiutendaji katika sekta hiyo.

2. Wizara iendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira pamoja na Kanuni za Maliasili Zisizorejesheka juu ya namna ya uchaguzi wa maeneo ya uchimbaji wa rasili mali hizo.

3. Wizara itafute njia bora na nafuu za uhuishaji na usimamizi mzuri wa maeneo yaliyochimbwa kifusi, mawe na mchanga.

4. Wizara iharakishe mchakato wa ombi la kampuni ya Zan Sand Co. Ltd ambayo inatarajia kutekeleza mradi wa kusaga mawe kwa ajili ya kutengeneza mchanga ili kusaidia upatikanaji wa rasilimali hiyo hapa nchini.

5. Serikali ihakikishe inalipatia ufumbuzi suala la magari ya Mchanga Taveta ili kuhakikisha wafanyabiashara hao wanafanya shughuli zao kwa utulivu na usalama na serikali nayo ikiokoa mapato yake.

6. Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha inanzisha inaanzisha Maabara ya Jiolojia ili iweze kutumika kufanya tafiti katika masuala ya nishati na madini.

7. Kamati inaishauri Wizara kuongeza wataalamu wa Madini ili kuleta ufanisi zaidi katika sekta hiyo.

## SEHEMU YA TATU

### 5:0 HITIMISHO

Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi inawapongeza kwa dhati Mawaziri, Makatibu Wakuu, Manaibu Katibu Wakuu pamoja Viongozi na watendaji wote kwa Ujumla wa Wizara zote tatu zinazosimamiwa na Kamati hii kwa mashirikiano makubwa waliyoipatia Kamati kwa kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake ya Kikatiba na Kikanuni.

Aidha, Kamati inatoa shukurani za kipekee kwa Maafisa Wadhamini wa Wizara hizi pamoja na wasaidizi wao wote kwa mashirikiano mazuri waliyoipatia Kamati wakati wote Kamati ilipokuwa Pemba katika kutekeleza majukumu yake.

Hata hivyo, kasoro kubwa iliyogunduliwa na Kamati ni **Upatikanaji wa fedha na kwa wakati na pia kwa kiwango kilichokadiriwa kutoka serikalini** kumekwamisha kwa kiasi kikubwa malengo na shabaha za Wizara zote tatu zinazosimamiwa na Kamati hii hasa katika miradi ya Maendeleo.

Vile vile, upatikanaji wa fedha za OC pamoja na vitendea kazi, uhaba wa wataalamu pamoja na usafiri navyo vimekuwa virejesha nyuma mwamko na ufanisi wa kazi.

Lakini pia ukosefu wa hati miliki katika majengo serikali pamoja na maeneo yake imekua ni changamoto kubwa na ya muda mrefu inayopelekea uvamizi na kusababisha migogoro.

### 5:1 MAPENDENDEKEZO NA USHAURI WA KAMATI KWA SERIKALI

- Kamati inaiagiza Serikali kuzipatia Wizara hizi fedha za Bajeti kwa wakati.

Vilevile, Kamati inatambua, kuthamini na Kushukuru ushirikiano mkubwa ilipata kutoka Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa kuweza kufanikisha ziara ya Kamati huko Tanzania na kujifunza Masuala ya Bandari na Mawasiliano. Aidha tunaishukuru Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi nayo kwa kutupeleka Shirika la Nyumba la Taifa huko Dodoma ili kuongeza uwelewa juu ya masuala ya maendeleo ya makaazi. Ziara zote hizo zilikuwa na manufaa makubwa ya kutuongeza uelewa na hatimae tuweze kuishauri vyema Serikali kupitia Sekta hizo.

Mwisho, Kamati inampongeza kwa dhati Spika wa Baraza la Wawakilishi Mhe. Zubeir Ali Maulid, Naibu Spika Mhe. Mgeni Hassan Juma, Katibu wa Baraza la Wawakilishi Ndg. Raya Issa Msellem, Afisa Mdhamini Afisi ya Baraza la Wawakilishi Pemba ndugu Abdulghani Abdullah Said na Mratibu wa Kamati Ndg. Khamis Hamad Haji pamoja na sekretariati yote ya Baraza la Wawakilishi kwa kuiwezesha vyema Kamati yetu kutekeleza majukumu yake na kuweza kutayarisha Ripoti yake kwa mwaka 2022/2023. Kamati inashauri mashirikiano hayo yaendelezwe kwa kipindi chote kinachofuata.